

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA TATU

29 OKTOBA, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA TATU – TAREHE 29 OKTOBA, 2026

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

36. MHESHIMIWA YAGI MAULID KIARATU (SINGIDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakarabati na kujenga upya Hospitali ya Manispaa ya Singida.

37. MHESHIMIWA HARAN NYAKISA SANGA (KIGAMBONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha mchakato wa kuifanya Dar es Salaam kuwa *Metropolitan Authority* ili kuiwezesha kuimarisha Sheria na Taratibu za Mamlaka hiyo.

38. MHESHIMIWA ANNE KILANGO MALECELA (SAME MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Shule ya Msingi Kitongoji cha Igoma Kata ya Maore katika Kijiji cha Mheza ambacho kipo jirani na Mbuga ya Mkomazi.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

39. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, upi mpango wa Serikali wa kuwaunganisha Kaya maskini na fursa nyingine za kujikwamua na umaskini badala ya kutegemea uwezeshaji mdogo wa TASAF.

WIZARA YA KILIMO:

40. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA (LULINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Bodi ya Korosho imepokea fedha kiasi gani inayotokana na *Export Levy* tangu kurejeshwa kwake na imetumikaje.

WIZARA YA FEDHA:

41. MHESHIMIWA CLAYTON REVOCATUS CHIPANDO (KIGOMA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha ukuaji wa uchumi unaonekana kwenye kipato cha Wananchi.

42. MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA (MAKETE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha Mamlaka ya kusimamia *Unclaimed Financial Assets* hapa nchini.

43. MHESHIWIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Bodi ya Bahati Nasibu ina mpango gani wa kudhibiti michezo ya kubahatisha (madugudugu ya Wachina) inayodaiwa kuharibu maadili nchini.

III. KAMATI YA MIPANGO:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028.

WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
29 OKTOBA, 2026**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**